UKIAMKA
«Umoja wa Kipentekoste Afrika
Mashariki na

THE HUB
Nordic Pentecostal Cooperation in Africa

SERVE

KUANDAA VIONGOZI WATUMISHI

Mafunzo ya Uongozi, Kiswahili
Toleo la pili

MAFUNZO YA UONGOZI KWA DHANA YA SERVE

Mpango wa kuandaa Viongozi Watumishi

Dhana ya mafunzo ya uongozi kwa jina la SERVE ni mpango wa mafunzo ya Kipentekoste wenye msingi wa kanuni 5 za kibiblia kuhusu kiongozi wa Kikristo. Kanuni hizo ni:

- Uongozi wa **KIROHO** - **S**PIRITUAL Leadership
- Uongozi wenye **UFANISI** - **E**FFECTIVE Leadership
- Uongozi wa **MAHUSIANO** - **R**ELATIONAL Leadership
- Uongozi wa **MAONO** - **V**ISIONARY Leadership
- Uongozi wa **KIUNJILISTI** - **E**VANGELISTIC Leadership

Dhana ya **SERVE** imetokana na kazi ya utafiti wa Dr Karl Inge Tangen wa Norway ambao ulifanyiwa kazi na wachungaji na viongozi toka nchi za **UKIAMKA**. Mwongozo huu wa mafunzo utatumiwa kuandaa viongozi chipukizi na wa sasa katika makongamano na makusanyiko ya ushirika na mtandao wa Umoja wa Kipentekoste Afrika Mashariki na Kati (**UKIAMKA)**.

Viongozi wa madhehebu ya **UKIAMKA** waliupitia mwongozo huu na kuukubali na kuuthibitisha ili uweze kutumika katika makanisa yote ya **UKIAMKA**. Hatua hiyo ilifanyika katika warsha ya viongozi hao iliyofanyika Nairobi Kenya mwezi May 2022.

YALIYOMO

MAANDIKO YA UTANGULIZI 4
FUNDISHO LA BIBLIA 4
YESU – KIONGOZI MTUMISHI 6
UONGOZI WA KIROHO 7
Lengo No.1: Kuwa mwanafunzi wa Yesu na kufuata kanuni zote za ufuasi wa Yesu katika maisha yake ya kila Siku. 7
Lengo No.2: Kuelewa Maana na umuhimu wa Wito katika Uongozi 8
Lengo No.3: Kuwaleta na Kuwaunganisha Watu kwa Kristo 9
UONGOZI WENYE UFANISI 10
Lengo No. 1: Kiongozi Mtumishi huishi Maisha ya Uwakili kama Biblia Inavyosema 10
Lengo No. 2: Mtumishi Kiongozi ana Uwezo wa Kusimamia Rasilimali kwa Ufanisi. 11
Lengo No. 3: Mtumishi Kiongozi ana Uwezo wa Kuwawezesha Wengine katika Masuala yote ya kijamii (Holistic Way) 12
UONGOZI WA MAHUSIANO 13
Lengo No. 1: Kutumika kwa Upendo, Hekima na Kuaminika 13
Lengo No. 2: Kukuza Watumishi viongozi. 14
Lengo No. 3: Kujenga Jamii yenye Haki na Amani 15
UONGOZI WA MAONO 16
Lengo No. 1: Kuwa na Ufahamu wa Maono Yanayotoka kwa Mungu. 16
Lengo No. 2: Kuwezesha Watu Kutafakari Kimkakati. 17
Lengo No. 3: Kuhamasisha Watu Kuleta Mabadiliko 18
UONGOZI WA KIUINJILISTI 19
Lengo No. 1: Viongozi Watumishi wana Uwezo wa Kuwasiliana na Jamii. 19
Lengo No. 2: Viongozi Watumishi wana Uwezo wa Kutumika na Kukidhi Mahitaji ya Jamii 20
Lengo No. 3: Viongozi Watumishi wana Uwezo wa Kushuhudia Upendo na Nguvu ya Kristo. 21
SHUKRANI 22

MAANDIKO YA UTANGULIZI

FUNDISHO LA BIBLIA

Katika Biblia tunaweza kuona mpango wa Mungu na kusudi la Mungu kwa ulimwengu. Ndani ya Biblia tunaona Mungu akitufundisha kuhusu uongozi.

UONGOZI WA KIROHO

"Sikia, ee Israel: Bwana Mungu wako ni Mungu mmoja. Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa nguvu zako zote. Amri hizi ninazokupa leo zitakuwa katika moyo wako. Wafundishe watoto wako kwa bidii. Nena kuhusu amri hizi uketipo nyumbani na wakati utembeapo njiani, ulalapo na uamkapo. Zifunge kama alama juu ya mkono wako, na uzifunge juu ya paji la uso wako. **Kum 6:4-8.**

- **Daudi kama kiongozi wa kiroho alijua kuwa yeye ni mtumishi wa Mungu 1 Sam 23:10-1; Zab 78:70-72.** *"Mtu anayeupendeza Moyo wa Mungu"* **1 Sam 13:14**. Hii ina maana kuwa kama kiongozi, alikuwa tayari kufuata mwongozo na maelekezo ya Mungu.
- **Daudi akawa na ujuzi wa kuabudu, kuimba, kutunga mashairi na nyimbo 2 Sam 6:14; Zab 3,9,11** +.
- **Daudi akawa kiongozi wa sifa na kuabudu 2 Nya 23:18.**
- **Daudi alikuwa na maono ya kujenga hekalu 1 Nya 28:2** lakini Sulemani ndiye aliyejenga hekalu hilo.

UONGOZI WENYE UFANISI

Musa aliambiwa kuwatumia watu wenye ujuzi mbalimbali ambao Mungu aliwajaza na Roho Mtakatifu kwa kazi mbalimbali katika kujenga hekalu. **Kut 35:30-35**. Ufanisi wa ibada kwa Mungu ilionekana katika ubora wa hekalu zuri lililojengwa kwa ustadi mkubwa na mavazi mazuri **Kut 28:31-35**, aina mbalimbali za muziki, nyimbo nzuri za aina mbalimbali na ustadi katika kutunga tungo na mashairi **Zaburi, Mithali, Isaya.**

- **Sulemani kama kiongozi mwenye ufanisi alisimamia miradi mikubwa miwili ya ujenzi** (Hekalu na jengo la makao ya kifalme)
- **Aliwawezesha wafuasi** wake kwa kufafanua majukumu na malengo katika muundo wa utawala /shirika lake. **1 Fal 4:2-6**
- **Alikuwa na mgawanyo wa majukumu na maeneo**. Aligawa wilaya kijiografia zikiongozwa na viongozi ambao nao walikuwa chini ya kiongozi mmoja. **1 Fal 4:7-19**
- **Aligawa rasilimali ndani na nje**. Kwa kushirikiana kiutawala na mfalme Hiram wa Tiro alifanya biashara ya chakula na mafuta kwa kubadilishana na idadi kubwa ya miti na mawe ya thamani **1 Fal 5:1-17**
- **Alipanga na kusimamia miradi mikubwa:** Sulemani aliweka watu 70,000 kubeba mizigo na 80,000 kuchonga mawe kwenye milima wakiongozwa na wasimamizi 3,600 waliosimamia kazi na kutatua matatizo ya kiutendaji na kuhimiza watu kutenda kazi. **2 Nya 2:2,18**.

UONGOZI WA KIMAHUSIANO

Uongozi wa kiroho uliendana na uongozi wa kimahusiano. Katika Torati, uhusiano wa mtu na Mungu ulikuwa lazima uendane na uhusiano na watu. Amri kumi zilikuwa ni msingi ambao ulifafanuliwa zaidi katika sheria ya Musa.

- **Utendaji katika kazi ya uongozi.** Umuhimu uliwekwa kwa miradi na watu. Sulemani kama kiongozi mwenye mahusiano aliwajali watumishi wake zaidi ya vile viongozi wengine walikuwa wakiwatendea watumishi wao. Alipanga zamu za watu 10,000 ili waweze kufanya kazi mwezi mmoja na wapumnzike miezi miwili ili waende kuangalia familia na mashamba yao. **1 Fal 5:13-14**

- **Kutatua migogoro na kusimamia sheria.** Mojawapo ya kazi ya mfalme (Kiongozi) ni kushughulikia migogoro kati ya watu akiwa kama mwamuzi. **1 Fal 3:16-28**. Hili lilifanyika kwa kugawa majukumu hayo kwa wazee walioketi katika lango la mji. **Rut 4:1-11**
- **Migogoro ya ndani, kugombea madaraka na mtandao wa kiutawala 1 Falm 1:1-30**. Nabii Nathani aliwasiliana na mama yake Sulemani Bath-sheba, akiwa na hofu kwamba lengo la Adoniya ni kumuua Solomon na mama yake.

UONGOZI WENYE MAONO

Biblia imejaa na mifano ya watu waliofuata maono yaliyotoka kwa Mungu.

- **Musa** "… maono ya nchi nzuri na kubwa, nchi iliyojaa maziwa na asali." **Kut 3:8**
- **Nehemiah** "… ili nikaujenge ukuta wa Yerusalem" **Neh 2:5**. "Haya na tuujenge ukuta wa Yerusalem." **Neh 2:17**.

UONGOZI WA KIUINJILISTI

Huu ni uhusiano wa nje kati ya kiongozi (watu wa Mungu) na watu wasioamini.

- **Kubadilisha mazingira ya kivita kuwa hali ya uhusiano wa kidiplomasia**
  Mungu alimwambia Daudi: "*Wewe hutajenga nyumba kwa ajili ya jina langu, kwa sababu umemwaga damu nyingi juu ya nchi machoni pangu. Tazama, utazaliwa mwana, atakayekuwa mtu wa kustarehe nami nitamstarehesha mbele ya adui zake pande zote; kwani jina lake litakuwa Sulemani, nami nitawapa Israel amani na utulivu siku zake."* **1 Nya 22:8-9**
- **Suleiman alifanya amani na kujenga mahusiano na watu wa mataifa mengine. 1 Fal 3:1**
  Sulemani alitoa zawadi na kutoa hekima yake kwa malkia wa Kushi na wafalme wengi. **1 Fal 4:34; 10:13**.

YESU – KIONGOZI MTUMISHI

Unyenyekevu – Kutoka hali ya Uungu na kuwa Mwanadamu.

- Yesu akajinyenyekeza bila kujali hali yake ya Uungu – **Flp 2:5-8.**

Yesu alionyesha nia ya utumishi

- Alikuja kutumika si kutumikiwa **Mt 20:28; Lk 22:27**.
- Alionyesha kwa mfano jinsi ya kuwa kiongozi mtumishi. **Yn 13:1-5**.

Yesu alitoa kipaumbele kwa watu - Alijali uthamani wa maisha yao.

- Alionyesha kuwahurumia watu na akawajali kila mmoja na hitaji lake kwa kuwasikiliza na kuwa na muda nao. **Mk 10:46-52: Yn 4:4-26; 12:1-7**.

YESU KAMA KIONGOZI WA KIROHO

- Alijazwa kwa Roho Mtakatifu na kudhihirisha tunda na karama za Roho Mtakatifu katika maisha yake. **Mt 3:13-17**.
- Alikuwa mtu wa Maombi akijenga uhusiano na baba yake. **Mt 14:23; Yn 4:1-3**.
- Tabia na mwenendo wake ulikuwa mkamilifu – hakuna mtu aliyemnyooshea kidole. **Mt 7:28-29; 27:54**.
- Aliwavuta watu kwake na kisha kuwaelekeza kuwa na uhusiano na Baba wa mbinguni. **Yn 15:1-17**.

YESU KAMA KIONGOZI MWENYE UFANISI

- Alifundisha kwa ufanisi mafundisho yenye kuleta mabadiliko katika maisha ya watu. **Mt 7:28-29**.
- Aliwaita na kuwafanya watu kuwa wafuasi (wanafunzi) wake. **Mk 3:13-15.**
- Alifafanua majukumu aliyowapa wanafunzi wake. **Mk 3:14-15; Lk 10:1-16; Mt 10:5-42**.
- Aliwawezesha wafuasi wake. **Yn 20:21-23**.
- Alisimamia kazi za wafuasi wake na kudai marejesho. **Mt 17:14-21**.
- Alihusika katika kutatua migogoro. **Yn 6:1-14**.

YESU KAMA KIONGOZI MWENYE MAHUSIANO

- Alionyesha upendo na huruma kwa watu. **Yn 11:32-36**.
- Alikuwa na muda wa kuwasikiliza watu na mahitaji yao. **Yn 4:1-26**.
- Alishughulikia mahitaji ya mtu binafsi si kundi peke yake. **Mk 10:46-52**.
- Aliwasaidia watu wenye mahitaji ya kimwili na kihisia. **Yn 5:1-9**.
- Alikuwa na uwezo wa kujenga timu – timu ya watu watatu, kumi na wawili, na sabini. **Lk 10:1-16**.
- Aliwajenga na kuwaimarisha watu – aliwaita wanafunzi wake kuwa naye kwanza kabla ya kuwatuma. **Mk 3:13.**
- Alikuwa mtu wa haki. **Yn 8:1-11**.

YESU KAMA KIONGOZI MWENYE MAONO

- Alikuwa na maono ya ufalme wa Mungu kwa sasa na kwa baadaye. **Mt 28:18-20; Mdo 1:8**.
- Alikuwa na maono ya viongozi kufanya kazi kwa umoja na kulijenga kanisa. **Mt 16:13-20**.
- Alitumia muda wake kuwekeza katika maisha ya watu. **Yn 15:1-17**.

YESU KAMA KIONGOZI MWINJILISTI

- Alifundisha na kuhubiri ujumbe usio na mchanganyiko na usiokuwa na unafiki. **Mt 5-7**; (**7:28-29**)
- Alikuwa mwinjilisti wa kuvuka mipaka ya tamaduni. **Yn 4:1-26; Mt 15:21-28**.
- Alikuwa na huruma kwa wenye dhambi na waliodharauliwa na jamii. **Mt 20:29-34**.
- Aliitwa rafiki wa wenye dhambi. **Mt 9:10-13; 11:18-19.**
- Alikuwa mtoaji mzuri wa mali zake na mwishowe akatoa maisha yake. **Mt 20:28**.

 UKIAMKA Copyright

UONGOZI WA KIROHO

Dira: Uhusiano kati ya kiongozi na Mungu.
Dhima: Viongozi wa Kikristo ni wale walio na uhusiano na Kristo, wakiwezesha neema ya Mungu kuonekana kupitia matendo ya wokovu na kuhusisha mambo yote yahusuyo uongozi mbele za Mungu.

Lengo No.1: Kuwa mwanafunzi wa Yesu na kufuata kanuni zote za ufuasi wa Yesu katika maisha yake ya kila Siku.

1.1 Kudhihirisha roho ya toba na kujitoa kumfuata Kristo kikamilifu.

1.1.1 Madhara ya dhambi, na umuhimu wa kujutia dhambi na kutubu.
- Kutengwa na Mungu - **Mwa 3; Isa 59:2; Rum 3:23**.
- Kuangamia – **Lk 13:1-5; Rum 6:23**.

1.1.2 Kuelewa neema ya Mungu na kazi ya Yesu msalabani.
- Neema ya Mungu kwa mtenda dhambi –**Efe 2:8; Ebr 2:9**
- Ukombozi – **Efe 1:7; Kol 1:13-14**

1.1.3 Maana ya kuwa mfuasi wa Yesu na kumfanya kuwa Bwana wa maisha (Ufuasi)
- Kuwa mfuasi wa Kristo - **Mt 16:24-26. Lk 9:23.**
- Kukaa ndani ya Kristo – **Yn 8:31; 15:1-17**

1.2 Kuwa na uhusiano wa dhati na Kristo kwa njia ya maombi na kusoma neno la Mungu kila siku.

1.2.1 Kukuza tabia za kiroho kama vile maombi na kufunga, kusoma neno la Mungu na kuabudu.
- Maombi na Kufunga – **Mt 6:5-18; 17:21; Efe 6:10-18; 1 The 5:17.**
- Kuabudu – **1 Nya 16:29; Zab 96:9; Yn 4:23-24**.
- Kusoma neno la Mungu – **Yn 8:31-32; 15:7; 2 Tim 3:16**

1.2.2 Kuwa na muda wa kutafakari neno na kumsikiliza Roho Mtakatifu
- Kutafakari – **Zab 1:2-3; 19:14; 119:23; Yos 1:8; 1 Tim 4:15.**
- Kumsikiliza Roho Mtakatifu – **Yn 16:13; Rum 8:14; Ufu 2:29**; **Gal 5:18**

1.2.3 Kuwa mshirika kamili wa kanisa la mahali
- Ushirika kwa kanisa **– Mdo 2:42; 1 Kor 1:9; 12:12**; **Efe 5:30.**

1.3 Kuonyesha maisha ya Kikristo, tunda la roho, na kuwa mfano wa Kristo.

1.3.1 Kuelewa hali mpya ya mtu aliye katika Kristo – Ni kiumbe kipya, mwana wa Mungu.
- Kuwa Kiumbe kipya – **2 Kor 5:17**
- Kuwa mtoto wa Mungu – **Yn 1:12; Gal 4:7; Flp 2:15; 1 Yn 3:1**

1.3.2 Kuelewa na kuishi kulingana na tunu za kikristo mfano Mahubiri ya Mlimani
- Tunu za Mkristo (Mahubiri ya Mlimani) – **Mat 5-7**

1.3.3 Kudhihirisha tunda la Roho Mtakatifu katika maisha
- Tunda la Roho – **Yn 15:16; Rum 7:4; Gal 5:22-23 Flp 1:11; Kol 1:10.**

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.

- **Swali:** Ni kwa njia gani kutengwa na Mungu kumeathiri maisha yetu na maisha ya watu wengine?
- **Tafakuri**: Ni tabia gani unazohitaji kuziishi ili kuboresha uhusiano wako na Kristo?
- **Hatua za kuchukua:** Tenga muda mbele za Bwana kila siku kwa maombi na kusoma neno la Mungu ili maisha yako yadhihirishe tunu za Ukristo na uweze kuzaa tunda la Roho Mtakatifu.

*Lengo No.2**: Kuelewa Maana na umuhimu wa Wito katika Uongozi***

2.1 Kutambua wito wa Mungu katika maisha ya mtu binafsi na wito huo kutambuliwa na viongozi wengine.

2.1.1 Kuelewa jinsi Mungu anavyomwita mtu
- Njia Mungu anazotumia kuita watu – **Mwa 12:1; Kut 3:4,10; Amu 6:14; 1 Sam 3:4; Isa 6:8; Mdo 13:1; 26:16.**

2.1.2 Kuelewa talanta na karama alizo nazo mtu binafsi
- Talanta - **Kut 31:1-11; 35:35; 38:23; 1 Fal 7:14**.
- Karama za Roho – **1 Kor 12; Rum 12:4-21; 2 Tim 1:6.**

2.1.3 Kuelewa umuhimu wa kutambuliwa na viongozi na kutii viongozi.
- Utambuliwa: **Hes 11:16; Mdo 13:1-3.**
- Utii kwa viongozi: **Ebr 13:7;17; 1 Pet 2:13.**

2.2 Kutambua na kuishi kulingana na sifa za kiongozi.

2.2.1 Kuelewa sifa za kiroho za mtumishi kiongozi
- Jinsi ya kuishi kulingana na sifa za kiroho za kiongozi - **1 Tim 3:1-13**

2.2.2 Kuonyesha tabia za kiroho katika maisha ya kila siku
- Kuwa na muda na Kristo – **Zab 55:17; Lk 2:37; 6:12.**
- Kutumika katika Roho – **Mik 3:8; Zek 4:6; Luk 4:14; Mdo 1:8; 4:33; 19:11-12.**
- Kuwa wakili mzuri wa rasilimali ulizopewa na Mungu – **1 Kor 4:1-2; 1 Tim 3:4; 6:20; 1 Pet 4:10.**
- Kukaa ndani ya Yesu – **Yn 15:4-10; 1 Yn 3:6**.

2.2.3 Kuishi kulingana na tunu za kiongozi
- Imani – **Ebr 11:6**
- Upendo – **1 Kor 13; 1 Pet 4:8**
- Tumaini – **1 Kor 13**
- Hekima ya kiroho – **Mit 4:6-7; Yak 1:5**
- Unyenyekevu – **Flp 2:3-8; 1 Pet 5:6-7**
- Uadilifu - **Mit. 11:3; 1 Kor 4:2.**

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali:** Unawezaje kuwasaidia Wakristo kugundua talanta zao na karama zao ili kuzitumia kwa ajili ya ufalme wa Mungu?
- **Tafakuri:** Tafakari kuhusu tabia 5 za uongozi na jinsi unaweza kuzitumia katika maisha yako ya kila siku.
- **Hatua za Kuchukua:** Orodhesha tabia za kiongozi na za kiroho unazotakiwa kuziboresha na chukua hatua ya kuboresha tabia hizo.

Lengo No.3: ***Kuwaleta na Kuwaunganisha Watu kwa Kristo***

3.1 Kuishi maisha ya Mfano – Kumfanana Kristo

3.1.1 Kuelewa na kueleza maana ya kuishi maisha ya mfano kwa wengine.
- Kuwa mfano –**2 Kor 3:3; Flp 3:17; 2 The 3:9; 1 Tim 4:12; Tit 2:7**.

3.1.2 Kufuata Mfano wa Kristo katika uongozi wa kitumishi
- Kumuiga Kristo – **Yn13:12-15; 1 Kor 11: 1; Flp 2:5-7.**

3.1.3 Kukuza nia ya kufanya kila kitu kama kumfanyia Mungu **Mt 25: 40; Kol 3:23.**

3.2 Kuwa na uwezo wa kufanya huduma kama vile kuhubiri, kufundisha kuongoza maombi, maombezi, kuabudu na kuto**a**.

3.2.1 Kuwa na uwezo wa kuandaa mahubiri na mafundisho yanayowaunganisha watu na Kristo.
- Kumhubiri Kristo kwa nia njema – **Flp 1:15-17; 2 Kor 2:17.**
- Kuhubiri ujumbe unaolingana na mazingira ya mahali: **Mdo 17:22-23.**

3.2.2 Kudhihirisha uwezo wa kuongoza maombi, maombezi kanisani na kuwatuma wale walioitwa katika huduma.
- Ongoza mikutano ya Maombi - **1 Kor 14:26; 1 Tim 2:1-3**.

3.2.3 Kuweza kuwaongoza watu katika kusifu na kuabudu pamoja na kutoa
- Ongoza timu ya kusifu na kuabudu - **2 Nya 5:13-14; Kol 3:16-17; 2 Kor 9:6-15**

3.3 Kuonyesha uwezo katika kuendesha ibada za ubatizo, ushirika, ndoa na kubariki watoto.

3.3.1 Kufahamu msingi wa kibiblia kuhusu ibada husika.
- Kufahamu kuhusu Agizo Kuu la Yesu na huduma za Kanisa **Mt 28:19-20; 1 Kor 11:23-34; Mt 19:5; Mk 10:13-16**.

3.3.2 Kufahamu mambo ya msingi katika kuendesha ibada hizo.
- Fuata miongozo ya kanisa katika kuendesha huduma za kanisa.

3.3.3 Kuwafundisha watu umuhimu wa ibada hizo.
- Rejea 3.3.1

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali:** Jadili jinsi unavyoweza kuishi maisha ya mfano isiyo maneno matupu.
- **Tafakuri:** Ni sifa/tabia gani zimekuwa za muhimu katika maisha ya kukua kwako katika Kristo?
- **Hatua za Kuchukua:** Tafuta watu katika huduma yako unaoweza kuwaongoza kuwa wafuasi/wanafunzi kamili wa Kristo ili waweze kukua kiroho**.**

UONGOZI WENYE UFANISI

Dira: Kuwa na uongozi wenye utendaji bora na wenye matokeo chanya
Dhima: Kuwa Mtumishi Kiongozi na wakili mzuri anayetunza na kutumia rasilimali vizuri na kwa ufanisi unaoleta mafanikio.

*Lengo No. 1**: Kiongozi Mtumishi huishi Maisha ya Uwakili kama Biblia Inavyosema***

1.1 Kuelewa na kuishi kulingana na kanuni za Biblia kuhusu uwakili.

1.1.1 Kuishi kulingana na kanuni za kibiblia kuhusu uwajibikaji.
- Kuwajibika mbele za Mungu - **Mwa. 1:28; 2:15; Rum 14:12; Ebr. 4:13**
- Kuwajibika mbele za watu - **Mt. 25:14-30**

1.1.2 Kueleza umuhimu wa mawasiliano katika uongozi
- Uwazi unaopelekea kuaminiwa – **Lk 19:17; Yn 15:15. Mdo 20:20-21**.
- Uwazi unatia moyo watu kushiriki/kuhusika

1.1.3 Kufanyia kazi kanuni za biblia kuhusu tathimini.
- Kujitathimini mwenyewe - **Omb 3:40; 2 Kor. 13:5; Gal 6:4.**
- Kutathiminiwa na watu wa nje - **Mt. 25:14-30**

1.2 Kudhihirisha umahiri na ujuzi wa usimamizi wa fedha.

1.2.1 Onyesha uwazi katika matumizi ya fedha.
- Kuwa mkweli mbele za Mungu na mbele za watu - **2 Kor 1:12-13; 8:20-22.**
- Kuwa mwaminifu kwa yale uliyokabidhiwa – **Mt 25:15-30; Lk 16:10; 1 Kor 4:1-2.**

1.2.2. Fanya mipango ya ukaguzi wa fedha.
- Fanya mipango ya ukaguzi - **Mt. 25:14-30**.

1.2.4 Tunza kumbukumbu vizuri.
- Simamia utunzaji wa kumbukumbu za rasilimali - **Mt. 25:14-30.**

1.3 Kuonyesha ujuzi katika usimamizi

1.3.1 Onyesha umakini na ubora katika kufanya kazi
- Kiwango chenye ubora - **Mwa. 1:1-12,18; Isa 41:7**

1.3.2 Onyesha umuhimu wa mchakato wa kazi kwa faida ya jamii,
- Fanya kazi kama kwa Bwana - **Efe. 2:10; Kol. 3:23.**

1.3.3 Onyesha utayari wa mabadiliko na uwezo wa kupokea mawazo mapya katika utendaji kazi.
- Kuwa wazi kwa mawazo mapya – **Mdo 16:6-10; 1 Kor. 9:22.**

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali:** Uwajibikaji unawezaje kuboresha ufanisi katika uongozi?
- **Tafakuri:** Ni kwa jinsi gani kushindwa kuwajibika kumeathiri uongozi wako? Mfano wa kujifunza: Nini kilitokea kwa mtu ambaye alishindwa kuwajibika kwa Bwana wake? **Mt 25:14-30.**
- **Hatua za Kuchukua:** Tafuta na fanyia kazi maeneo ambayo unahitaji kuimarisha uwajibikaji wako.

Lengo No. 2: ***Mtumishi Kiongozi ana Uwezo wa Kusimamia Rasilimali kwa Ufanisi.***

2.1 Weka mipango ya shughuli kwa wakati uliopangwa.

2.1.1 Zingatia umuhimu wa muda na fedha katika kupanga mipango
- Kupanga mipango - **Mit 21:5; Lk 14:28.**

2.1.2 Weka kipaumbele cha shughuli na watu katika mchakato wa mipango.
- **Amu 7:4: Efe. 4:11-12; Lk 6:12-16; 10:1.**

2.1.3 Weka malengo na vipaumbele
- **Mit 6:8; 22:3; 24:27; Lk 12:33**.

2.2 Zingatia umuhimu wa muundo wa uongozi na kuutimia ipasavyo.

2.2.1 Weka muundo wa uongozi unaoeleweka wazi.
- **Kut 18:17-25**.

2.2.2 Andaa na weka watu katika kazi kulingana na nafasi na ujuzi wao
- **Mdo 6:1-4; 1 Kor. 3:6; Efe. 4:11-12.**

2.2.3 Andaa kanuni na miongozo bora
- Rejea muundo na sera za kanisa/shirika lako.

2.3 Dhihirisha umahiri katika kutambua na kutumia rasilimali kwa ufanisi

2.3.1 Tambua vyanzo vya rasilimali
- **Kut 35:4-28; Yoh 6:1-15; Mat. 17:27; 1 Kor 16:1-2.**

2.3.2 Fuata kanuni za matumizi sahihi ya rasilimali
- **Mhu. 11:1-2; Yn 6:12; Zab 90:12.**

2.3.3 Tunza na kuangalia rasilimali watu na rasilimali nyingine.
- **Mwa. 2:15; Mk 6:31; Mdo 20:28.**

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali**: Elezea umuhimu wa muundo wa uongozi katika kanisa/shirika lako.
- **Tafakuri:** Ni kwa njia gani umetumia kanuni za kibiblia katika kuwaweka watu katika nafasi zao sahihi?
- **Hatua za Kuchukua:** Tambua njia zinazoweza kusaidia katika kutafuta na kutumia vema rasilimali katika huduma yako.

Lengo No. 3: ***Mtumishi Kiongozi ana Uwezo wa Kuwawezesha Wengine katika Masuala yote ya kijamii (Holistic Way)***

3.1 Gawa majukumu na kufafanua wajibu

3.1.1. Kutafuta uongozi wa Mungu katika kuweka watu kwenye huduma
- **Mdo 13:1-4; Mt 9:37-38.**

3.1.2 Kuwawezesha watu na kuwapa nyenzo za kutumia.
- **Efe. 4:12; Ebr. 13:20-21; Neh. 4:16-17**

3.1.3 Kufafanua majukumu na wajibu
- **Mdo 6:3; 1 Kor 12; Efe 4:11-12.**

3.2 Wafundishe na kuwalea (mentor) wengine katika uongozi na kuwasaidia kuwa bora kwa maeneo mbalimbali ya uongozi

3.2.1 Kufunza na kuinua watumishi viongozi
- **Mdo 20:18-21; 1 Kor 4:16; Flp 4:9; 1 The 1:6; 2 Tim. 2:1-2, 1 Tim. 1:1-3**

3.2.2 Kuweka mpango wa kulea viongozi (mentorship)
- **Mk 3:13-14; 2 The 3:9; 1 Tim 4:12; Ebr 6:12; 13:7,17.**

3.2.3 Kuwaandaa viongozi na kuwapa stadi za maisha
- **Yn 13:1-17; Mdo 20:20-21; 2 Tim. 1:13; Tit 2:7.**

3.3 Fahamu umuhimu wa kukaimisha madaraka na wajibu

3.3.1 Unda makundi na kuyapa majukumu.
- **Mdo 6:1-7.**

3.3.2 Tengeneza nafasi za kazi na kuwapa kazi za kufanya
- **Kut 18:25; Tit 1:5.**

3.3.3 Simamia kwa kuangalia ubora wa kazi
- **Mdo 15:36-41.**

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali:** Ni kwa njia gani unawafunza na kuwalea viongozi katika huduma yako?
- **Tafakuri:** Changamoto gani umekutana nazo katika kuwa na mpango wa kulea viongozi katika huduma yako?
- **Hatua za Kuchukua:** Ainisha maeneo katika huduma yako ambayo unapaswa kukaimisha majukumu yako kwa njia nzuri.

 UKIAMKA Copyright

UONGOZI WA MAHUSIANO

Dira: Watu na Mahusiano
Dhima: Mtumishi Kiongozi anatumika kwa upendo, hekima na kuaminika, na kuinua watumishi viongozi wengine ili kujenga jamii ya haki na amani.

*Lengo No. 1**: Kutumika kwa Upendo, Hekima na Kuaminika***

1.1 Kudhihirisha Upendo katika kumtumikia Mungu na watu

1.1.1 Elezea jinsi ya kuonyesha upendo unapomtumikia Mungu na watu
- Amri kuu – **Mt 22:37-39, 1 Yn 3:11**.
- Upendo wa Mungu – **Yn 3:16; 13:35; 15:12; 1 Yn 4:7-12.**

1.1.2 Onyesha jinsi ya kuonyesha upendo unapomtumikia Mungu na watu
- Upendo & Huduma – **Efe 4:2-3, Yn 15:13; Rum12:9; 1 The 3:12; 1 Pet 1:22.**
- Uwe Mtumishi – **Yn 13:1-17, Lk 22:23-27, Mt 20:28, Mk 10:45**.

1.2 Kutenda kwa hekima katika kumtumikia Mungu na watu.

1.2.1 Elezea hekima ya kiroho na ufahamu unaotokana na neno la Mungu na mafundisho sahihi ya neno la Mungu
- Omba hekima –**Yak 1:5; 1 Fal 3:9; Zab 119:169; Mit 2:1-4.**
- Fundisha mafundisho sahihi – **Kum 32:2; Mit 4:2; Kol 1:28-29; 3:16; 1 Tim 4:6; 2 Tim 3:14-17; Tit 1:9-10; 2:1-15.**

1.2.2 Onyesha hekima ya kiroho katika kumtumikia Mungu na watu
- Kuwa na Hekima katika kuhukumu - **Flp 1:9-11; 1 Fal 3:9, 16-28; Ebr 5:14.**
- Kuwa na hekima katika mahusiano – **Yak 3:13-18.**

1.3 Kuishi maisha ya imani kwa Mungu ili kuweza kuaminiwa na wafuasi.

1.3.1 Fafanua mambo yahusuyo maisha ya kumwamini Mungu
- Imani ya kuwa Mungu huwatunza watu wake - **Mt 6:31-34; Zab 9:10, Yer 17:7; Lk 12:7; Zab 115:12; 1 Pet 5:7.**

1.3.2 Elezea dhana ya kuaminiwa na watu
- Tumeaminiwa hivyo tunatakiwa kuwaamini wengine. - **Mt 25:20, 1 Tim 6:20; 2 Tim 2:2.**

1.3.3 Onyesha jinsi ya kumwamini Mungu na watu.
- Kuamini watu kimatendo - **Zab 55:17; 37:3,5; 118:8; Mit 3:5.**

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali:** Upendo, Hekima na Kuamini watu kunaweza kujidhihirisha namna gani unapomtumikia Mungu na watu?
- **Tafakuri:** Nini unachofikiri kinakosekana katika maisha yako cha kukuwezesha kumtumikia Mungu na watu kwa upendo, hekima na kuamini watu?
- **Hatua za Kuchukua:** Ainisha mabadiliko unayohitaji katika maisha yako ili uweze kumtumikia Mungu na watu kwa upendo, hekima na imani.

 UKIAMKA Copyright

Lengo No. 2: ***Kukuza Watumishi viongozi.***

2.1 Dhihirisha uongozi wa utumishi kwa kuishi maisha ya mfano

2.2.1 Elezea umuhimu wa kuwa kiongozi wa mfano.
- Viongozi wanapaswa kuwa mfano –1 Kor 11:1, 1 Tim 4:12, Tit 2:6-7, 1 Pet 2:16, 1 Pet 2:12, Filp 3:17,

2.2.2 Elezea aina (model) ya uongozi wa kitumishi aliouonyesha Yesu
- Yesu alikuja kutumika - Yoh 13:1-15, Yoh 13:15, Yoh 20:21, Mat 5:16

2.2.3 Ongoza kama mtumishi kiongozi
- Jinsi kiongozi mtumishi alivyo – Luk 17:10, Matt 7:15-20, Gal 5:22

2.2 Onyesha kuwa unawaamini watumishi wenzako kwa kuwasikiliza na kuwafuatilia.

2.2.1 Eleza umuhimu wa kuwasikiliza na kuwafuatilia kama njia ya kuwatia moyo.
- Kwa nini ni muhimu kuwasikiliza, kuwafuatila, na kuwatia moyo wengine? – Mat 9:36-38, Yoh 11:33-35, Mat 25:14-30, Efes 3:20.

2.2.2 Onyesha namna ya kusikiliza, kuwa na watu na wakuwatia moyo watumishi wenzako
- Nguvu ya kutia moyo watu - Mat 25:31-45, Yoh 3:17, Gal 6:2, Ebr 3:13, Ebr 6:18, Ebr 10:24-25.

2.3 Onyesha uongozi wa utumishi kwa kufanya kazi pamoja

2.2.1 Eleza dhana ya kiongozi mtumishi kufanya kazi kwa umoja
- Mwili mmoja katika Kristo – 1 Kor 12, Efs 4:4-6, Mark 3:24, Rum 12:4, Zab 133:1, Yoh 13:35

2.2.2 Onyesha jinsi ya kufanya kazi pamoja kama watumishi viongozi
- Kuchukuliana mizigo - Gal 6:2, Ebr 13:6, Mat 5:41-42, Rum 12:13, Yak 2:14-17, Efes 4:16.

2.2.3 Onyesha masuala yahusuyo kulea, kushauri na kufunza viongozi wapya
- Yesu & Petro – Luk 5:1-11, Luk 22:32, Joh 21.
- Paulo & Timotheo & Tito – 1&2 Tim, Mdo 16.
- Prisila, Akila & Apollo – Mdo 18:26.
- Barnaba & Paulo – Mdo s 9:27, 11:25-26.
- Eliya & Elisha – 1 Fal 19:19-21, 2 Fal 2.
- Yethro and Musa - Kut 18:39.
- Yoshua –Kumb 31:23.

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali:** Ni kwa njia gani unaweza kuwa mfano kwa wengine, huku ukiwatia moyo na kufanya kazi pamoja nao?
- **Tafakuri:** Nani amekuwa kiongozi wa mfano kwa maisha yako? Ni kwa njia gani umetiwa moyo na kusaidiwa na kiongozi mwenye mahusiano?
- **Hatua za Kuchukua:** Tambua mabadiliko yanayohitajika katika maisha yako yatakayokuwezesha kuwa mfano mzuri kwa wengine ili watiwe moyo na kufanya kazi pamoja nawe.

Lengo No. 3: ***Kujenga Jamii yenye Haki na Amani***

3.1 Kuweka mipaka salama na kuzuia tabia zinazoweza kuharibu tabia ya kiongozi.

3.1.1 Elezea dhana na umuhimu wa kuwa na mipaka katika mahusiano
- Kulinda tabia njema – Mwa 1-3, Yak 4:12, Mith 25:17, Efes 6:4, Gal 5:13-15.
- Kujilinda na ubaya - 2 Kor 6:14, Rum 12:2, Zab 37:27.

3.1.2 Elezea jinsi ya kuweka mipaka salama
- Ufahamu & Hekima – Mith 3:7, Ayub 27:6, Ayub 28:28, Zab 34:11-14, Yak 1:16,

3.1.3 Onyesha jinsi ya kujilinda na tabia mbaya zinazoweza kuharibu huduma
- Jenga tabia njema 1 Tim 4:6-11, Mith 4:23-27, Eph 4:25-32, Rum 8:5-6.

3.2 Onyesha jinsi ya kutafuta amani na upatanisho

3.2.1 Fafanua na elezea mchakato wa kutafuta amani na upatanisho
- Mchakato wa kuleta upatanisho na amani – Kol 1:20-22; 2 Kor 5:18

3.2.2 Elezea umuhimu wa kutafuta amani na upatanisho
- Umuhimu wa amani na upatanisho – Ebr 12:14; Rum 5:8-11.

3.3 Tunza na kuza tabia ya kuaminika

3.3.1 Elezea umuhimu wa kujenga utamaduni wa kuaminiana
- Ujasiri mbele za Mungu na wengine - Yoh 14:1; 1 Kor 11:1.

3.3.2 Eleza umuhimu wa kuwa na utamaduni wa kuaminiana
- Hamasisha ujasiri ndani ya watu – Isa 12:2.

3.3.3 Jenga utamaduni wa kuaminiana katika mazingira ya kazi
- Kutiana moyo – Isa 41:7; 1 Thess 5:11.

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali:** Ni kwa njia gani unaweza kuwatia moyo watu kutunza mipaka ya mahusiano?
- **Tafakuri:** Unaweza kukumbuka tukio katika huduma yako ambapo mgogoro ulitokea na jinsi ulivyoushughulikia na kuleta amani na upatanisho?
- **Hatua za Kuchukua:** Tambua maeneo ambayo unaweza kuyatumia kuwatia moyo wengine ili wawe na ujasiri.

UONGOZI WA MAONO

Dira: Kutambua ni wapi tunakoenda na kwa nini.
Dhima: Mtumishi Kiongozi ana uwezo wa kuelezea maono aliyopewa na Mungu na kuwawezesha watu kutambua mikakati na kuhamasika ili kuleta mabadiliko kulingana na maono ya Mungu.

Lengo No. 1: ***Kuwa na Ufahamu wa Maono Yanayotoka kwa Mungu.***

1.1 Tafuta, tambua na elewa maono yanayotoka kwa Mungu

1.1.1 Elezea jinsi ya kutafuta na kupokea maono kutoka kwa Mungu
- Maono hupelekea mtu kumtafuta Bwana - **Mit 29:18; Mdo 3:1-8; 9:1-12.**

1.1.2 Elezea sifa ya maono kutoka kwa Mungu.
- Huthibitishwa na wengine – **Mdo 13:1-3.**
- Humtukuza Mungu.**Yn 16:14-15.**
- Hueneza Ufalme wa Mungu. **Mt 9:36-38**
- Hupelekea kuwasaidia wengine.

1.2 Fahamu jinsi ya kuwasilisha maono yaliyotoka kwa Mungu

1.2.1 Elezea jinsi ya kuwasilisha maono uliyopewa na Mungu (kutegemea unayewasiliasha kwake)
- Wasilisha maono kama ulivyopokea badala ya kutoa tafsiri yako. **Mdo 11:1-18.**

1.2.2 Tambua muda mwafaka wa kuwasilisha maono kutoka kwa Mungu
- Muda mwafaka na njia mwafaka – Mfano yaliyomkuta Yusufu.

1.3 Onyesha hamasa kwa maono yanayotoka kwa Mungu

1.3.1 Hamasa kwa nguvu ya Roho Mtakatifu - **Yer 20:9; Mdo 26:19**
1.3.2 Jenga hamasa kwa mambo yanayoleta utukufu kwa Mungu. **Hes 14:5-9.**

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali:** Kwa nini ni muhimu maono kutoka kwa Mungu kuthibitishwa na wengine?
- **Tafakuri:** Ni maono ya jinsi gani ulipokea wakati Bwana alipokuita?
- **Hatua za Kuchukua:** Elezea maono yako kwa maandishi.

Lengo No. 2: ***Kuwezesha Watu Kutafakari Kimkakati.***

2.1 Wezesha watu kutafakari kimkakati kuhusu maono

2.1.1 Wezesha watu kuelewa maono kwa kutumia neno la Mungu.
- **Mdo 15:1-17**

2.1.2 Linganisha maisha ya Ukristo na namna nyingine za ibada.
- **Mdo 17:16-32.**

2.2 Kuza maono yako ya huduma ukilinganisha na maono ya Ufalme wa Mungu na maono ya kanisa lako

2.2.1 Elezea jinsi maono ya ufalme wa Mungu ni kutoka vizazi hadi vizazi
- **Mwa 12:1-3; Zab 145:4; Dan 4:3.**

2.2.2 Dhihirisha nafasi ya Ujumbe wa Ufalme wa Mungu kwa masuala ya mazingira
- **Mwa 1:26-28, 2:15; Neh 9:6**

2.3 Jenga tabia ya kutafakari kimkakati mara kwa mara.

2.3.1 Jenga utaratibu wa kuwasiliana mara kwa mara, kukumbushia na kuangalia upya maono kama yanatimizwa
- Mfano wa Paulo kutembelea makanisa na kukumbushia maono kwa njia ya waraka. Mdo 15:36.

2.3.2 Elezea umuhimu wa kuendelea kukumbushia na kutafakari kuhusu maono.
- Wafanye watu waishi kwa mwelekeo wa maono hayo. 2 Pet 1:12.

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali:** Elezea Maono ya ufalme wa Mungu kwa kuzingatia masuala ya mazingira.
- **Tafakuri:** Ni mapokea gani yamepotosha mafundisho ya msingi wa imani katika huduma yako?
- **Hatua za Kuchukua:** Weka mkakati wa kutunza mazingira katika eneo la huduma yako**.**

Lengo No. 3: ***Kuhamasisha Watu Kuleta Mabadiliko***

3.1 Himiza watu kuwa vyanzo vya kuleta mabadiliko

3.1.1 Eleza kuwa mtumishi kiongozi ni mtu ambaye anaendelea kubadilishwa kwa nguvu ya Roho Mtakatifu.
- **1 Sam 10:6; Rum 12:2.**

3.1.2 Sisitiza umuhimu wa mabadiliko yanayoanzia kwa mtu binafsi
- **Mk 3:13-14.**

3.1.3 Wezesha watu kujitathmini wenyewe kuhusu uongozi wa kiutumishi
- **Mt 7:1-5; Omb 3:40; 2 Kor 13:5.**

3.2 Onyesha ubunifu na mabadiliko

3.2.1 Hamasisha watu kuwa wabunifu kubuni njia na mikakati mipya.
- **Mak 1:38.**

3.2.2 Fafanua umuhimu wa kuchambua kwa undani mapokeo kwa kulinganisha na imani mpya/ mawazo mapya na mikakati mipya
- **Isa 43: 19; Efe 4:14-15**

3.3 Ongoza kuleta mabadiliko kwa hekima.

3.3.1 Eleza kuwa maono hayawezi kufikiwa bila msaada wa Mungu na watu wengine ambao wameitwa na Mungu
- **Mdo 11:25-26**

3.3.2 Shughulikia upinzani kwa hekima kupitia mazungumzo na ushirikishwaji.
- **Mdo 15:1-11**

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali:** Ni changamoto gani umepitia katika kuleta mabadiliko, njia na mikakati mipya?
- **Tafakuri:** Ni kwa njia gani umefanyika kuwa chombo cha mabadiliko katika huduma yako?
- **Hatua za Kuchukua:** Anzisha mjadala wa kuleta mabadiliko katika maeneo ambayo unaona yanahitaji mabadiliko.

 UKIAMKA Copyright

UONGOZI WA KIUINJILISTI

Dira: Kuwa na maisha yenye ushuhuda unaoaminika na unaoleta utukufu kwa Kristo
Dhima: Watumishi viongozi wanawezesha kanisa kuonyesha upendo wa Mungu kwa jamii kwa njia ya kushirikiana, na kutumika kwa nguvu ya Roho Mtakatifu.

*Lengo No. 1: **Viongozi Watumishi wana Uwezo wa Kuwasiliana na Jamii.***

1.1 Kuelewa umuhimu wa kuwasiliana na kushirikiana.

1.1.1 Eleza maana ya kufanya mawasiliano na kushirikiana na watu (connecting and network.)
- Fuata Mfano wa Yesu – mawasiliano na Zakayo (**Lk 19:2**), Mwanamke Msamaria (**Yn 4**), Watoza ushuru (**Mt 9:10**); - aliitwa rafiki wa wenye dhambi.

1.1.2 Onyesha njia mbalimbali za kuwasiliana na watu
- Urafiki, ukaribu na kujihusisha na kazi za jamii

1.1.3 Tafuta njia za kushirikiana na watu kwa maeneo mbali mbali.
- Urafiki, ukarimu na kushiriki kazi za jamii
- Kanisa kuungana na mashirika mengine.

1.2 Kushirikiana na wenye mamlaka.

1.2.1 Tambua na kuheshimu mamlaka mbalimbali
- **Rum 13:1; Kut 22:28; Mdo 23:5; 1 Pet 2:17.**

1.2.2 Tafuta njia za kushirikiana na wenye mamlaka
- Shirikiana katika masuala ya kisheria na serikali – **Neh 2:4-8**
- Shirikiana katika masuala ya maendeleo ya jamii

1.3 Kuwa na majadiliano ya kutafuta ufumbuzi mwafaka wa changamoto katika jamii.

1.3.1 Uwe na mahusiano na jamii kwa kushiriki katika kazi za jamii
- Mfano wa programu za maji, afya, elimu n.k.

1.3.2 Tumia mbinu za kutatua migogoro katika jamii
- Jihusishe na utetezi na mijadala ya kimaendeleo katika jamii. Mfano Hekima ya Solomoni kwa wanawake wawili wenye watoto. – **1 Fal 3:16-28.**

1.3.3 Himiza moyo wa kuwa na usawa katika kanisa.
- **Yak 2:1-5; 1 Kor 1:10-15.**

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali:** Jadili njia mbalimbali za kushughulikia migogoro
- **Tafakuri:** Ni kwa njia gani kushirikiana na kujiunganisha na watu/mashirika kumekuwa ni muhimu kwako.
- **Hatua za Kuchukua:** Tafuta kundi au shirika unaloweza kushirikiana na kujiunganisha nalo.

Lengo No. 2: ***Viongozi Watumishi wana Uwezo wa Kutumika na Kukidhi Mahitaji ya Jamii***

2.1 Kuelewa na kukidhi mahitaji ya watu na kuombea mafanikio yao.

2.1.1 Sikiliza kwa makini mahitaji ya watu katika jamii.
- Fuata Mfano wa Yesu – Mgonjwa kwenye kisima (**Yn 5:1-10**); Bartimayo kipofu. (**Mk 10:46-52**).

2.1.2 Tafiti mahitaji ya watu katika jamii
- Habari ya Nehemia ya kutafiti mahitaji yaliyokuwepo **Neh 2:11-18**.
- Yesu katika kuwalisha maelfu – **Mt 14:13-21**.

2.1.3 Panga na endesha maombezi
- **Yer. 29:7; Mt 9:35-38.**

2.2 Onyesha ukarimu kupitia huduma na upendo kwa wageni.

2.2.1 Dhihirisha ujuzi wako wa kijamii. (Huruma kwa watu)
- **Math 25:34- 40.**

2.2.2 Ishi maisha ya kiutumishi kama Biblia inavyoeleza
- **Gal 6:9; Mt 24:45.**

2.2.3 Uwe mkarimu kwa wageni na wasioamini
- **Heb 13:2; Kum 10:19.**

2.3 Ishi kwa vitendo kuhusiana na masuala ya maendeleo kwa maeneo yote ya mwanadamu

2.3.1 Anzisha mipango ya kimaendeleo inayogusa mahitaji ya watu katika jamii
- **2 Kor 8:1-15**

2.3.2 Himiza mipango ya utunzaji mazingira.
- **Mwa 1:28; 2:15**

2.3.3 Jihusishe na mipango ya kijamii katika maeneo yako.
- **Mdo 6:1-7**

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali:** Ni kwa njia gani kazi za jamii zinaweza kusaidia kueneza Injili?
- **Tafakuri:** Jadili jinsi kanisa linavyoweza kubarikiwa kwa kukaribisha wageni na wasioamini katika kanisa.
- **Hatua za Kuchukua:** Tathmini mahitaji ya sasa katika jamii yako.

 UKIAMKA Copyright

Lengo No. 3: ***Viongozi Watumishi wana Uwezo wa Kushuhudia Upendo na Nguvu ya Kristo.***

3.1 Kuhubiri Injili ya Yesu Kristo

3.1.1 Kuwa na muda wa kusoma neno la Mungu kwa ajili ya kufundisha
- **2 Tim 2:15; Yos 1:8; Ezr 7:10.**

3.1.2 Kutumia stadi za kuhubiri na kufanya kazi za Uinjilisti
- **2 Kor 4:1-2; 2:17; Isa 58:1; 62:1; 1 Tim 4:6.**

3.1.3 Kutoa ushuhuda wako kwa watu
- Fuata mfano wa Petro na Paulo walivyotoa ushuhuda kwa waliowashitaki.

3.2 Kutendea kazi karama za Roho na kudhihirisha nguvu ya Kristo

3.2.1 Onyesha umuhimu wa karama za roho katika kuonyesha upendo wa Yesu
- **1 Kor 12 & 13.**

3.2.2 Onyesha nguvu ya Kristo kupitia maisha yako.
- **Mk 9:23-24; 16:17-18; Lk 17:6; Yn14:12; 2 Kor 12:9-10.**

3.2.3 Kuwa na mazoea ya kuomba na kufunga.
- **Efe 6:18-20; Mk 9:28-29.**

3.3 Kuwafikia watu wa tamaduni tofauti – (Umisheni)

3.3.1 Tuma wamishonari kwa tamaduni tofauti
- **Mt 28:18-20.**

3.3.2 Wafanye watu kuwa wanafunzi wa Yesu na kukua kuwa kama Yesu.
- **Kol 1:28-29; Efe 4:11-16.**

3.3.3 Tambua nguvu ya ushirika katika kuanzisha makanisa.
- **Mdo 2:42-47; Ebr 10:24-25.**

Swali, Tafakuri, na Hatua za Kuchukua.
- **Swali:** Jadili njia potofu za kiuinjilisti zilizopo katika jamii yako.
- **Mjadala:** Ni kwa njia gani kanisa lako linajihusisha kuhubiri injili katika jamii yako na watu wa tamaduni tofauti?
- **Hatua za Kuchukua:** Panga mipango ya kufanya kazi ya injili kwa watu wa tamaduni tofauti.

SHUKRANI

Viongozi wafuatao kutoka nchi 13 za madhehebu ya **UKIAMKA** wamefanya kazi ya kuwezesha kutoa mafundisho haya ya SERVE katika mazingira ya Kiafrika.

1. Jackson Joseph Kaluzi	FPCT, Tanzania
2. Christopher Osuka	FPFK, Kenya
3. Tamirat Tariku Ashebir	Guenne, Ethiopia
4. Sanbeto Bashe	EHBC, Ethiopia
5. Leweyehu Sineshaw	FGBC, Ethiopia
6. James Lado	SPC, South Sudan
7. Godfey Wafula	PCU, Uganda
8. Aimabe Nsabayesu	ADPR, Rwanda
9. Murithi Imathiu	FGCK, Kenya
10. Nicolas Hakizimana	CPEBU, Burundi
11. Biringanine Rukumeza	CELPA, Congo
12. Assan Biruli	CEPAC, Congo

PENTECOSTAL CHURCHES OF UGANDA
Reaching Nations For Christ

Communauté des Eglises de Pentecôte au Burundi
CEPBU

የኢትዮጵያ ሙሉ ወንጌል አማኞች ቤተክርስቲያን
ጽ/ቤ - ደቡብ ሱዳን

GUENET

fpfk

PENTECOSTAL MINISTRIES OF UGANDA CHURCHES
CALLED TO CARE

ADEPR

CELPA

የኢትዮጵያ የሕይወት ብርሃን ቤተ ክርስቲያን
YEHIWOT BERHAN CHURCH OF ETHIOPIA

FULL GOSPEL CHURCHES OF KENYA

The Free Pentecostal Church of Tanzania
FPCT

SUDAN PENTECOSTAL CHURCH
(SPC)

CEPAC
Communauté des Eglises de Pentecôte en Afrique Centrale

UKIAMKA
East and Central Africa Pentecostal Association(ECAPA)